JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

Simu Nambari: 2152532/3
Fax Na: 2152820
*(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe kwa Kamishna wa Mamlaka )*

08 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 80327,
**DAR ES SALAAM.**

# TAARIFA KWA UMMA

UDHIBITI NA MAPAMBANO YA DAWA ZA KULEVYA KWA MWAKA 2019

**01 January 2020. Dar es Salaam:**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inawashikilia watu wawili kwa tuhuma za **KUSAFIRISHA DAWA ZA KULEVYA. Watu hao ni ABUU SALEHE KIMBOKO** mfanya biashara na mkazi wa Mbagala, Dar es Salaam na **PASCAL PETER LUFUNGA**, mkazi wa Bwilingu KIBAHA Mkoa wa PWANI

**ABUU SALEHE KIMBOKO** alikamatwa tarehe 29 Desemba 2019 katika eneo la **Mbagala Zakiem / Mpakani,** akiwa na dawa za kulevya aina ya heroin gramu 400 pamoja na bastola moja na risasi za moto kumi tano vyote vikiwa kwenye gari **lenye namba za usajili T568 DKC TOYOTA SPACIO** ambalo alikutwa akiliendesha.

Mtuhumiwa wa pili **PASCAL PETER LUFUNGA** alikamatwa katika nyumba anayoishi huko Bwilingu KIBAHA akiwa na dawa za kulevya aina ya Heroin yenye uzito wa gramu 133.33. Watuhumiwa wote wanatarajiwa kufikishwa mahakamani mapema iwezekanavyo.

Vilevile katika kipindi cha mwaka wa 2019, Mamlaka imefanya Operesheni mbalimbali na kufanikiwa kukamata dawa za kulevya kiasi cha kilo 325.69 za bangi zikiwahusisha

watuhumiwa wawili (2); kilo 892.24 za mirungi zikiwahusisha watuhumiwa tisa (9); na kilo 34.47 za Heroin zikiwahusisha watuhumiwa watano(5).

**Kwa upande wa Kesi za dawa za kulevya,** Kesi 35 zimemalizika katika Mahakama Kuu na dawa zilizohusika na kesi hizo zimeshateketezwa. Aidha, ifahamike kuwa pale ambapo Jamhuri haikuridhika na maamuzi au adhabu iliyotolewa kwa washitakiwa wa dawa za kulevya haikusita kukata rufaa. Kwa mfano, Jamhuri imekata rufaa Mahakama Kuu ya Tanzania kupinga adhabu ya faini ya Shilingi million 1 aliyopewa **MUSTAFA JUMA KHAMIS** na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya kumtia hatiani kwa kosa **la kukutwa na** dawa za kulevya aina ya heroin gramu 40.16 ndani ya chumba chake. Msingi wa rufaa ya Jamhuri ni kwamba **kiasi cha fine alichotozwa mtuhumiwa hakiendani na adhabu mbadala ya kifungo cha miaka 30 jela.**

**Vilevile, mwaka 2019,** Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mashtaka ya Taifa (NPS), imefanikiwa kushinda mashauri kadhaa makubwa ya dawa za kulevya. Miongoni mwa mashauri hayo ni lile lilohusu kilo 63 za Heroin ambalo iliendeshwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara. Ambapo watuhumiwa MWINYI KITWANA RAJABU NA ALLY HAMDUNI HAMAD walihukumiwa kifungo miaka 20 jela na kutaifisha **gari iliyohusika kusafirisha dawa za kulevya.**

Pia katika shauri lililohusisha raia 12 wa Iran wakiwa na Boti MV AL-IMRAN waliokamatwa tarehe 01 mwezi Februari mwaka 2018, Mahakama Kuu ya Tanzania iliwatia hatiani washitakiwa wote kwa kosa la kuwa na dawa ya kulevya aina ya bangi iliyisidikwa ( HASHISH) pamoja na kufanya shughuli za uvuvi katika maji ya Tanzania bara bila kibali. Washtakiwa wote kwa pamoja waliadhibiwa kulipa fidia Serikali kiasi cha shilingi za kitanzania **milioni 100** pamoja na kulipa faini ya shilingi milioni moja kila mmoja. Vilevile mahakamani iliamuru kuutaifishwa kwa **JAHAZI** na kuwa mali ya serikali.

**Katika shauri dhidi ya** wakurugenzi na wafanyakazi wa kampuni ya **TECHNO NET SCIENTIFIC** ambalo lilihusu uingizaji wa kemikali bashirifu isivyo halali, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliwaamuru washitakiwa Benedict Gabriel Assey na wenzake sita (6)

kulipa fidia ya shilingi milioni mia moja (100) na faini ya shilingi laki tano kila mmoja kwa kosa la kujihusisha na biashara ya kemikali bila kuwa na usajili.

**Kwa mwaka 2019 tuliteketeza Dawa za Kulevya mara mbili.** Mwezi Agosti 2019 ziliteketezwa kilo 1.65 za Heroin na gramu 547.21 za Cocaine katika kiwanda cha Saruji jijini Mbeya na mwezi Oktoba, 2019 jumla ya kilo 120.90 za Heroin na kilo 70.96 Cocaine ziliteketezwa katika kiwanda cha saruji cha Twiga kilichopo Wazo Hill jijini Dar es salaam.

**Kwa upande wa Tiba na Kinga** tumefungua kituo kingine cha kutibu waathirika wa dawa za kulevya cha Itega Dodoma. Pia tumekamilisha ujenzi wa vituo vya Tiba vya Bagamoyo na Kibaha na ujenzi wa kituo cha Tanga unaendelea. Mpaka sasa vituo vinavyotoa tiba ya **Methadone** kwa waathirika wa dawa za kulevya aina ya heroin ni sita ambavyo ni Muhimbili, Mwanayamala na Temeke vya Dar es salaam; Hospital ya rufaa Mbeya na Hospitali ya Rufaa ya Sekou Toure, Mwanza na Itega Dodoma.

**Pia kuna Nyumba za upataji nafuu; (sober house)** ambazo zinasimamiwa na asasi za kiraia, ambapo ziko jumla nyumba 30. katika mikoa 11 zillizopo; Dar es Salaam, Pwani , Mwanza, Iringa, Tabora, Kilimanjaro, Morogoro, Arusha, Tanga, Kagera na Dododma.

Waraibu wanao tibiwa katika vituo na nyumba za upataji nafuu wanapata elimu ya jinsi ya kutosambaza magonjwa yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya (eg. Kifua kikuu, homa ni aina ya B na C na maambukizi ya VVU.) amabyo yanaweza kuleta madhara katika jamii.

**Elimu:**

Tumewafikia watu wengi na kutoa Elimu juu ya madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya, wengi hawajiingizi na wanawachukia wauzaji na wanatoa tarifa kwetu, hali hii imepunguza uwepo wa dawa za kulevya mitaani na watumiaji wanaozagaa hovyo barabarani.

**Aidha** Mamlaka imefanikiwa kudhibiti matumizi yasiyo sahihi ya Kemikali bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya kulevya. Kwa kutoa elimu imetolewa kwa wazalishaji,

wasambazaji wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya na wafanyabiashara wa Kemikali bashirifu kuhusu ushirikiano unaotakiwa ili kudhibiti biashara hii haramu.

**Kumekuwa na** Changamoto nyingi katika udhibiti dawa za kulevya. Kuogezeka kwa udhibiti wa dawa za kulevya kumefanya watumiaji kutumia dawa za tiba zenye asili ya kulevya kama mbadala wa dawa za kulevya.

**Pia**, wafanyabiashara wa dawa za kulevya wanabuni mbinu mpya kila mara, mfano hivi karibuni tuligundua wafanyabiashara wa dawa za kulevya aina ya Mirungi, wamekuwa wakisafirisha dawa hizo katika mfumo wa majani makavu, na kuipa majina bandia kama **Mlonge**, **Green tea** au **Dawa**.

Kwa mwaka huu tumejipanga Kuongeza nguvu katika kujenga vituo vingi ili kuwafikia waathirika wengi zaidi. Tunaendelea kuwakumbusha Watanzania wote kutambua tatizo la dawa za kulevya kuwa ni mtambuka hivyo tunahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali pamoja na Jamii kwa ujumla. Hivyo basi naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba Umma kwa ujumla wake kushiriki kwa dhati kabisa katika kukabiliana na tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini, Hasa kuwafichu wauzaji wa dawa za kulevya.

**Imetolewa na,**

Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**